HESLB NEWSLETTER

Toleo Na 2 Julai - Desemba 2012

# Mafanikio katika urejeshaji mikopo ya wanafunzi Tanzania

NA VENERANDA MALIMA

Kuna mambo mawili muhimu ya kuzingatia katika masuala ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu: moja, ni jinsi ya kuipata, na pili ni namna kurejesha mikopo hiyo muda unapowadia. Katika maana halisi; Urejeshaji mikopo ni kulipa kiasi cha fedha alichokopeshwa mtu kwa masharti fulani. Hiki ndicho kinachotokea kwa wanafunzi wa elimu ya juu ambao hukopeshwa fedha na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa ajili ya kugharamia masomo yao katika kipindi wanachokuwa vyuoni.



*Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Bodi wakishiriki katika mkutano uliofanyika Oktoba 20, 2012 katika Hoteli ya Oceanic Bay Resort, Bagamoyo.*

Tangu kampeni za urejeshaji mikopo zilipoanza mwaka 2007, kumekuwa na mafanikio makubwa katika ukusanyaji wa madeni kutoka kwa wanufaika wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Na hadi kufikia Juni 2012, asilimia 53 ya fedha zilizokopeshwa na ambazo zilikuwa zimeiva kwa ajili ya kurejeshwa zilikuwa zimeshakusanywa.

Makala hii inaelezea historia ya utoaji mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu nchini Tanzania na pia inaonyesha mwenendo wa ukusanyaji wa madeni hasa kwa kuangalia mafanikio yaliyofikiwa katika urejeshwaji wa mikopo hadi kufikia mwezi Juni 2012.

Dhana ya uchangiaji wa gharama za elimu ya juu bado haijaeleweka vizuri hapa nchini kutokana na ukweli kwamba kabla ya miaka ya 1990, huduma zote za kijamii ikiwa ni pamoja na elimu ya juu zilikuwa zikilipiwa au kutolewa bure na Serikali au wananchi walikuwa wakilipa kiasi kidogo sana. Baadaye mwelekeo ulibadilika kutokana na Programu za kurekebisha miundo ya kiuchumi zilizopendekezwa na Benki ya Dunia (WB) na Shirika la Fedha Duniani (IMF) mwishoni mwa miaka ya 1980 ili kupunguza matumizi ya serikali katika huduma za jamii na kuanzisha uchangiaji wa gharama za huduma hizo. Kuanzishwa kwa Bodi ya Mikopo ya

indelea uk. 3

## YALIYOMO

Mafanikio katika Urejeshaji Mikopo Ya Wanafunzi Tanzania.................. 1

Mchakato wa Maombi ya Mikopo Mwaka 2012/2013..................... 5

Uendelevu wa Mikopo ya Wanafunzi Nchini Tanzania ..... 7

Dondoo Za Kuvutia................... 8

Kupandishwa Vyeo na Uhamisho wa Wafanyakazi...... 9

Menejimenti ya Bodi Yakaribisha Wafanyakazi Wapya.......................................10

Kumbukumbu ya Voster Prosper Mariki......................... 10

# Ujumbe kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji

Toleo hili la pili la Jarida la HESLB limelenga zaidi katika masuala ambayo yalitokea katika kipindi cha miezi sita iliyopita katika maeneo mawili ya utoaji mikopo na urejeshaji wa mikopo kutoka kwa wanufaika wa mikopo hiyo.

Toleo hili limeandika habari za kipindi chenye majukumu mengi, wakati ambapo vyuo vilikuwa vinaanza mwaka mpya wa masomo na kukaribisha maelfu ya wanafunzi wapya. Pia ni kipindi ambacho Bodi ilifanya kazi kubwa ya kuhakikisha kuwa mwaka wa masomo unaanza vizuri kwa kuchambua mikopo kwa wakati na kuipeleka vyuoni kwa ajili ya wanafunzi stahiki.

Bodi inatoa shukrani za dhati kwa jitihada na ushirikiano wa wote waliohusika hususan Maafisa Mikopo, viongozi wa serikali za wanafunzi na uongozi wa taasisi za elimu ya juu.



*Bw. George R.W. Nyatega*

Suala la msingi ni kwamba Bodi imeendelea kujizatiti kwa ubora na kasi ya utoaji huduma zake.

Bodi ilifungua mchakato wa maombi ya mikopo mwezi Aprili 2012 ili kuwezesha wanufaika watarajiwa wa mikopo hiyo kutuma maombi yao na pia kuruhusu wanafunzi wanaoendelea na masomo kuhakiki uhitaji wao wa kuendelea kupatiwa mikopo. Tuna furaha kwamba wanafunzi walio wengi waliomba mikopo kwa mara ya kwanza na wanaoendelea na masomo walifuata utaratibu huo na kuwasilisha maombi yao ndani ya muda uliopangwa.

Kutokana na ukweli kwamba baadhi ya Wanafunzi hawakutuma maombi ya mikopo ndani ya muda, tunachukua fursa hii kwa mara nyingine tena kusisitiza umuhimu wa kuzingatia tarehe ya mwisho ya kutuma maombi ya mkopo. Zaidi ya hayo, tunawasisi waombaji na wadau wengine kufuatilia vigezo na masharti ya utoaji wa mikopo.

Tunatoa wito kwa wanufaika wa mikopo ambao tayari wamehitimu masomo yao, na muda wa kurejesha mikopo umewadia, wachukue hati za madeni yao na kuanza kurejesha kwa hiyari. Kwa moyo huu tutawezesha mfuko wa mikopo ya wanafunzi kuwa endelevu.


**Limechapishwa na:**
Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi
wa Elimu ya Juu,
S.L.P 76068,
Dar es Salaam, Tanzania
Simu: 255 22 2669036/7
Faksi: 255 22 2669039
Barua pepe: info@heslb.go.tz
Tovuti: www.heslb.go.tz

Bw. George Nyatega – Mhariri Mtendaji
Bw. Cosmas Mwaisobwa – Mhariri Mkuu
Bi. Veneranda Malima – Mhariri
Dkt. Henry Mambo - Mshauri

**Wachangiaji**
Bw. Daud Maneno
Bi. Eline Maronga
Bw. Sunday Charles
Bi. Joyce Mgaya

**Usanifu na Uchapishaji**
PenPlus Ltd.


# Kutoka kwa Mhariri

Karibu katika toleo la pili la jarida la HESLB. Toleo hili limesheheni mkusanyiko wa habari zilizojiri kwenye Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu katika kipindi cha miezi sita iliyopita tangu toleo la kwanza lilipochapishwa.

Toleo la kwanza la jarida hili lilipokelewa vizuri na wasomaji wetu. Tunawashukuru wote waliotumia muda wao kusoma na kututumia maoni yao na wengine waliolazimika kuomba nakala zaidi kutokana na kuongezeka kwa mahitaji.

Wakati tunaandaa toleo hili, tulizingatia umuhimu wa masuala husika ambayo yalionekana ni vema kushirikishana. Kwa mantiki hiyo,



*Bw. Cosmas Mwaisobwa*

tunakaribisha habari au picha ambazo zinafaa kuchapwa katika jarida hili.

Ni matumaini yangu kwamba yaliyomo katika toleo hili yataendelea kuwa ya kuelimisha na kuhabarisha.

inatoka uk. 1

Wanafunzi wa Elimu ya Juu ni matokeo ya sera ya serikali ya uchangiaji wa gharama za huduma za jamii katika miaka hiyo ya 1990, ambapo moja ya mikondo ya sera hiyo ilikuwa ni sera ya kuchangia gharama za elimu ya juu. Sera hii iliandaliwa na kupangwa kutekelezwa katika awamu tatu. Awamu ya kwanza ilianza kutekelezwa mwaka 1992/93 ambapo wanafunzi walitakiwa kujilipia gharama za usafiri kwenda chuoni na kurudi nyumbani, gharama za usajili pamoja na michango ya serikali za wanafunzi. Pia gharama za maombi, gharama za matibabu, gharama za mitihani na fedha za tahadhari. Gharama hizi zilikuwa ni ndogo na kila mwanafunzi aliweza kuzimudu.

Utekelezaji wa awamu ya pili ulihitaji mwanafunzi pamoja na kuchangia gharama zilizoainishwa katika awamu ya kwanza, alipaswa pia alipie gharama za chakula na malazi. Gharama hizo zilikuwa kubwa kwa wanafunzi walio wengi na hivyo Serikali ilianzisha utaratibu wa mikopo. Utaratibu huu ulianza kutumika mwaka 1994/1995 na uliendelea kutumika hadi mwaka 2004/2005.

Awamu ya tatu ilianza kutekelezwa mwaka 2005/2006 baada ya kuanzishwa kwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu. Awamu ya tatu inamtaka mwanafunzi agharamie pamoja na gharama zilizotajwa kwenye awamu ya kwanza na ya pili na gharama za masomo, mahitaji maalum ya vitivo, mafunzo kwa vitendo na utafiti ama kwa njia ya mkopo kutoka kwenye Bodi hii au kutoka vyanzo vingine.

## Utoaji mikopo kuanzia mwaka 1994/1995 hadi 2011/2012

Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu inaweza kugawanywa katika sehemu mbili tangu ilipoanzishwa mwaka wa masomo 1994/1995. Sehemu ya kwanza ni wakati mikopo ilipokuwa ikitolewa moja kwa moja na Serikali kupitia Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia hadi Juni, 2005. Sehemu ya pili ni kuanzia Julai, 2005 Bodi ilipoanza utendaji hadi sasa. Idadi ya wanafunzi wanaokopeshwa na kiasi cha fedha zinazotolewa kwa wanafunzi husika imekuwa ikiongezeka kutoka mwaka mmoja wa masomo hadi mwingine kama inavyooneshwa katika jedwali 1(a).

**Jedwali 1(a) Takwimu za Utoaji Mikopo kuanzia Julai 1994/1995 hadi 2011/2012**

| Mwaka wa Masomo | Idadi ya Wanafunzi waliokopeshwa | Kiasi kilichokopeshwa (Sh Bilioni) |
|---|---|---|
| **Mikopo iliyotolewa na serikali** | | |
| 1994/1995 to 2004/2005 | 48,378 | 51,103,685,914 |
| **Jumla ndogo** | 48378 | 51,103,685,914 |
| **Mikopo iliyotolewa na Bodi** | | |
| 2005/2006 | 42,729 | 56,111,371,483.00 |
| 2006/2007 | 47,554 | 76,071,839,629.00 |
| 2007/2008 | 55,687 | 110,873,883,141.00 |
| 2008/2009 | 58,798 | 139,093,681,094.00 |
| 2009/2010 | 72,035 | 197,348,958,875.00 |
| 2010/2011 | 92,791 | 231,855,927,151.85 |
| 2011/2012 | 94,773 | 322,031,207,695.73 |
| **Jumla ndogo** | 464,367 | 1,133,386,869,069.58 |
| **JUMLA KUU** | 512,745 | 1,184,490,554,983.58 |

Jumla ya kiasi cha fedha kilichokopeshwa kwa wanafunzi wa elimu ya juu kati ya Julai, 1994 na Juni, 2012 inafikia **Tzs 1,184,490,554,983.58,** ambapo kati ya kiasi hicho **Tzs 51,103,685,914.00** zilitolewa na Wizara ya Elimu Juu, Sayansi na Teknolojia na **Tzs 1,133,386,869,069.58** zimetolewa na Bodi tangu ilipoanza rasmi shughuli za utendaji Julai 2005.

## Urejeshaji mikopo hadi kufikia Juni 30, 2012

Baada ya mwanafunzi mnufaika kuhitimu masomo yake, hupewa muda wa mwaka mmoja wa kujiweka sawa (grace period) kabla ya kuanza kurejesha mkopo. Anapoanza kurejesha, hufanya hivyo kwa awamu kwa kiasi ambacho kinakuwa kimeiva kwa ajili ya kurejeshwa kwa mwezi.

Takwimu za Urejeshaji Mikopo hadi kufikia Juni, 2012 zinaonyesha kuwa kiasi kinachorejeshwa kwa awamu na makusanyo yake kutoka kwa wanufaika yanaendelea vizuri.

- Katiya **Tzs. 1,184,490,554,983.58** zilizokopeshwa kati ya Juni, 1994 na Juni, 2012, ni kiasi cha **Tzs. 160,730,886,339.00** ndicho kimeiva kwa ajili ya kurejeshwa kutoka kwa walengwa walionufaika na mikopo ya wanafunzi katika kipindi hicho wapatao **110,529**.
- Kiasi kilichobaki cha **Tzs. 1,023,759,668,644.58** bado hakijaanza kurejeshwa kutokana na sababu kwamba wanafunzi ambao wamenufaika na mikopo hiyo ama wanaendelea na masomo au bado wako katika kipindi cha mwaka mmoja wa kujiweka

endelea uk. 4

inatoka uk. 3

sawa (grace period).

- Aidha, kati ya kiasi cha mikopo ambayo ilikuwa imeiva na hivyo kuwa tayari kurejeshwa, ni mikupuo yenye thamani ya jumla ya **Tzs. 39,539,748,704.85** ndiyo ilipaswa kuwa imekusanywa hadi kufikia Juni, 2012**.**

Hadi Juni, 2012 kiasi cha **Tzs 20,153,923,234.24** kilikusanywa kutoka kwa wadaiwa **a**mbacho ni sawa na **53%** ya **Tzs. 39,539,748,704.85** ambazo zilikuwa tayari kwa ajili ya kukusanywa kutoka kwa walengwa.




**Kielelezo Na. 1: Mwenendo wa Urejeshwaji Mikopo kuanzia 2006/2007 hadi 2011/2012**

## Changamoto za urejeshaji mikopo ya wanafunzi

Licha ya mafanikio ambayo yamepatikana katika kipindi cha miaka 5 iliyopita tangu urejeshaji wa mikopo ya wanafunzi ulipoanza, kumekuwa pia na changamoto kadhaa ambazo Bodi imekabiliana nazo.

Changamoto ya kwanza ya ugumu wa kuwapata wanufaika inayochangiwa kwa kiasi fulani na wanufaika wengi kutokuwa na anuani za makazi au kutotoa taarifa sahihi za sehemu wanakofanya kazi iwapo wameajiriwa au wanakofanyia shughuli zao binafsi iwapo wamejiajiri.

Changamoto ya pili inatokana na Utamaduni wa kutokuwa na utayari wa kurejesha mikopo kwa wakati miongoni mwa wakopaji na inasababisha wanufaika walio wengi kuamini hawapaswi kurejesha mikopo iwapo hawatatafutwa na kutakiwa kufanya hivyo na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu.

Ushirikiano mdogo kutoka kwa baadhi ya Waajiri pia imekuwa changamoto. Hali hii imepunguza kasi ya utambuzi wa wanufaika na hata ukusanyaji wa makato ya madeni pia kufanyika kwa kasi ndogo.

Licha ya changamoto hizo, Bodi imeweka mikakati ya kuwasiliana na waajiri ili kuwaelimisha juu ya umuhimu wa kuwasilisha majina ya waajiriwa wao walionufaika na mikopo ya wanafunzi ili waanze kufanya marejesho mara tu wanapoajiriwa. Vile vile Bodi inatumia Mawakala wa kukusanya madeni (Debt Collectors) kwa lengo la kuwatafuta wanufaika nchi nzima ambao hawajajitokeza ili warejeshe fedha walizokopeshwa. Mawakala hao pia wana jukumu la kukusanya marejesho ya mikopo kutoka kwa wanufaika.

**Jedwali 1(b) Mwenendo wa Urejeshaji Mikopo kuanzia Julai 2007 hadi Juni 2012**

| Mwaka wa Masomo | Makusanyo kwa Mwaka | Makusanyo ya Jumla |
|---|---|---|
| 2006/2007 | 53,616,011.00 | 53,616,011.00 |
| 2007/2008 | 858,941,262.29 | 912,557,273.29 |
| 2008/2009 | 1,176,404,180.00 | 2,088,961,453.29 |
| 2009/2010 | 2,147,075,264.78 | 4,236,036,718.07 |
| 2010/2011 | 4,409,171,729.99 | 8,645,208,448.28 |
| 2011/2012 | 11,508,714,785.96 | **20,153,923,234.24** |

## Mikakati ya kuongeza kasi ya urejeshaji mikopo ya wanafunzi

Ili kuongeza kasi ya Urejeshaji wa mikopo ya wanafunzi, Bodi imeweka mikakati kuanzia mwaka wa fedha 2012/2013 kama ifuatavyo:

- Kushirikiana na taasisi wadau ili kuwapata wanufaika ambao hawajaanza kurejesha mikopo yao. Taasisi wadau ni pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Wizara ya Fedha (Hazina), Ofisi ya Takwimu ya Taifa, Tume ya Mipango n.k.
- Kutumia Ofisi za Serikali za Mitaa kuwatafuta wanufaika
- Kushirikiana na Kitengo cha Uhamiaji katika Wizara ya Mambo ya Ndani kwa ajili ya kuwakumbusha wanufaika ambao hawajaanza kurejesha mikopo wanaokwenda nje ya nchi
- Kuboresha Mfumo wa urejeshaji mikopo unaotumika kwa sasa ili kuwa na taarifa za kutosha za

endelea uk. 5

inatoka uk. 4

wanufaika wote

- Kukagua na kutembelea ofisi za waajiri ambako wanufaika wa mikopo wameajiriwa ili kuona kama hitaji la kuwasilisha majina ya wanufaika linatekelezwa au la.
- Kuongeza urejeshaji mikopo kwa njia ya simu za mkononi
- Kuhakikisha wanafunzi wanufaika wanapata hati ya mikopo wanayodaiwa kwa njia ya mtandao
- Kuitumia kikamilifu Sheria ya Bodi kuhusu Urejeshaji Mikopo.
- Kutuma bure ujumbe mfupi wa simu za mkononi kutoa taarifa za hiari kuhusu mahali waliko wanufaika
- Kuendelea kutumia wakala wa kukusanya madeni

### Hitimisho

Kila mdau wa elimu ya juu ana jukumu muhimu la kufanikisha urejeshaji wa mikopo. Wanufaika wa mikopo wana wajibu mkubwa zaidi katika kuhakikisha mikopo yao inarejeshwa haraka na kwa hiyari. Waajiri, Wadhamini, Wazazi/Walezi na Umma kwa ujumla wana wajibu wa kuhakikisha mikopo inarejeshwa na hivyo kujenga mfuko endelevu wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu.

Bila mikopo ya wanafunzi ingekuwa vigumu kwa wanafunzi wengi kumudu gharama za elimu ya juu. Kutokana na hilo, ni muhimu kwa wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu na wadau wote kuzingatia taratibu za urejeshaji wa mikopo ili kuwezesha urejeshwaji mzuri wa mikopo katika miaka ijayo.

---

# Mchakato wa Maombi ya Mikopo Mwaka 2012/2013

NA JOYCE MGAYA NA ELINE MARONGA

Aprili 16, 2012 ulikuwa mwanzo wa mchakato mwingine wa maombi ya mikopo ambapo Bodi ya Mikopo ya Wananfunzi wa Elimu ya Juu kwa mara nyingine tena ilifungua milango kwa waombaji wa mikopo ya Wanafunzi. Hata hivyo, kabla ya kujaza fomu za maombi kwa njia ya mtandao, kulikuwa na nyaraka mbili muhimu ambazo waombaji walipaswa kuzielewa vizuri; wa kwanza ulikuwa ni mwongozo na vigezo vya utoaji mikopo na ruzuku kwa mwaka wa masomo 2012/2013 na wa pili ulikuwa ni mwongozo wa maombi ya mkopo kwa njia ya mtandao. Nyaraka zote mbili zilitangazwa sana na zilikuwa zimewekwa kwenye tovuti ya Bodi www.heslb.go.tz na pia kulikuwa na vipeperushi ambavyo vilichapishwa na kusambazwa katika taasisi za elimu ya juu, Posta za wilaya na Ofisi za Maafisa Elimu wa Wilaya.

## Sifa na Vigezo

Vigezo vya ustahiki havikubadilika. Kama inavyobainishwa katika Sheria ya Bodi, mwombaji lazima awe Mtanzania, awe ameomba mkopo kwa njia ya mtandao (OLAS), awe amedahiliwa kwa masomo ya muda wote (full time) katika chuo kinachotambulika kwa ajili ya Shahada ya kwanza au Stashahada ya Juu na asiwe amefadhiliwa na taasisi au chanzo kingine cha fedha.

## Mchakato wa Maombi

Waombaji walipaswa kulipa ada ya Tsh. 30,000 kupitia huduma ya M-Pesa na kupatiwa nambari ya kumbukumbu ambayo ingetumika kujisajili katika mtandao. Baada ya hapo walipaswa kujiandikisha kwenye mtandao kupitia anuani ya (http://olas.heslb.go.tz) kwa kuchagua kundi la mwombaji, kujaza fomu kama ilivyoelekezwa, kuchapisha fomu iliyokamilika, kuambatanisha nyaraka husika zilizokuwa zimeorodheshwa, na kisha kupeleka fomu kwa Hakimu/Mwanasheria au Serikali ya Kijiji/Mtaa kwa ajili ya kuthibitishwa. Hatimaye kila mwombaji alitakiwa kutuma kifurushi cha maombi ya mkopo kilichokamilika kwa njia ya huduma ya kutuma vifurushi kwa haraka (EMS) kwenda Ofisi za Bodi. Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ilikuwa Juni 30, 2012.

## Makundi ya waombaji na Nyaraka za kuambatanisha

Kwa ujumla kulikuwa na Makundi 3

endelea uk. 6



*Viongozi wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi za Tiba cha Mt. Fransisi (SFUCHAS) wakisikiliza maelezo yaliyokuwa yanatolewa na Afisa wa Bodi aliyekuwa ametembelea Chuo hicho Desemba 10, 2012.*

inatoka uk. 5

ya waombaji wa mikopo.

**(i) Waombaji wa mara ya kwanza: Shahada ya kwanza (ndani na nje ya nchi)**
Kwa ajili ya uthibitisho, waombaji walipaswa kuambatanisha nyaraka kadhaa ikiwa ni pamoja na cheti cha kuzaliwa au "affidavit" kwa ajili ya uthibitisho wa uraia, vyeti vya kifo kwa ajili ya uthibitisho wa uyatima/ mzazi mmoja, barua ya Daktari kwa ajili ya ulemavu, barua rasmi ya kustaafu kwa mzazi, vivuli vya vyeti vya taaluma vilivyothibitishwa na kivuli cha kitambulisho cha mpiga kura au pasi ya kusafiria ya mdhamini.

**(ii) Waombaji wa mara ya kwanza: Shahada za Uzamili na Uzamivu (ndani na nje ya nchi)**
Waombaji wa mara kwanza wa Shahada za Uzamili na Uzamivu wanapaswa kuwa wahadhiri katika vyuo vya elimu ya juu vinavyotambulika na wanapaswa wawe wameteuliwa na mwajiri na kuidhinishwa rasmi kabla ya kutuma maombi ya mkopo.

**(iii) Wanafunzi wanaoendelea na masomo: Shahada ya kwanza, Uzamili na Uzamivu (nchini na nje ya nchi)**
Waombaji katika kundi hili walipaswa kujaza ukurasa mmoja wa fomu ili kuthibitisha uhitaji wao wa kuendelea kupokea mikopo ya Wanafunzi.

## Vipengele vya Mkopo

Bodi inatambua kuwepo kwa gharama nyingi katika masomo ya elimu ya juu lakini inalenga kutoa mikopo katika maeneo yafuatayo: chakula na malazi, vitabu na viandikwa, mahitaji maalum ya vitivo, mafunzo kwa vitendo, utafiti na ada ya mafunzo.

## Kozi za Vipaumbele vya Taifa

Kutokana na mahitaji makubwa ya mikopo ya Wanafunzi dhidi ya ufinyu wa bajeti, kwa mwaka wa masomo 2012/2013, Wanafunzi waliodahiliwa kusoma katika kozí zilizotajwa hapa chini watapewa kipaumbele:-

- Ualimu - Sayansi na Hisabati
- Sayansi - Tiba (Udaktari wa Binadamu, Udaktari wa Wanyama, Upasuaji wa Meno, Tiba za Wanyama, Ufamasia na Uuguzi)
- Uhandisi - Ujenzi na Umwagiliaji
- Ualimu - Masomo yasiyo ya Sayansi au Hisabati (kupitia king'amuzi uwezo)
- Uhandisi (fani zinazotambuliwa na Bodi za Usajili wa Wahandisi ikiwa ni pamoja na Uhandisi wa Kompyuta na Usanifu wa Majengo (kupitia king'amuzi uwezo)
- Sayamsi za Kilimo (kupitia king'amuzi uwezo)
- Sayansi za Wanyama (kupitia king'amuzi uwezo)

Mikopo ikiidhinishwa inatumwa kwa vyuo husika na baada ya hapo wanafunzi hupatiwa mikopo yao kupitia akaunti za Benki baada ya taasisi husika kujiridhisha na usajili wa Wanafunzi wake na ufaulu wa kitaaluma.

Waombaji waliofanikiwa kupata mikopo lakini hawakuridhika na kiasi cha mkopo walichopangiwa, wanaweza kukata rufaa mara baada ya vyuo kufunguliwa na wanapatiwa siku 90 kutuma maombi yao ya rufaa.

## Maombi ya Mkopo kwenye Mtandao

Idadi ya waombaji wa mikopo wa mara ya kwanza waliojiandikisha kupitia mfumo wa kuomba mikopo kwa njia ya mtandao (OLAS) kwa mwaka wa masomo 2012/2013 walikuwa 47,928, idadi ambayo ilikuwa juu ya makadirio ya Bodi iliyokuwa waombaji wa mara ya kwanza wapatao 38,600. Mfumo huu ambao umekuwa ukitumiwa na waombaji mikopo wa mara ya kwanza na wanaoendelea na masomo wa hapa nchini na nje ya nchi katika miaka miwili ya masomo 2011/2012 na 2012/2013, umekuwa njia muafaka ya mchakato wa kuomba mikopo ya Wanafunzi. Kwa msaada wa vipeperushi na taarifa zilizokuwa zimewekwa kwenye tovuti ya Bodi, waombaji waliweza kujaza kwa urahisi fomu za maombi kwa mtandao.

## Dawati la Msaada

Katika mwaka wa masomo 2012/2013, Bodi imeajiri maafisa wa dawati la msaada kwa wateja chini ya Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano (IEC), lengo ni kuwa na mawasiliano mazuri na wadau wake. Katika kipindi cha maombi ya mkopo, maafisa wa dawati la msaada walijibu simu kutoka kwa waombaji wa mikopo ambao walikutana na matatizo wakati wa kujaza fomu kwenye mtandao. Kitengo cha IEC kwa kushirikiana na kitengo cha TEHAMA vilifanya kazi pamoja hususan katika masuala ya kiufundi ili kuhakikisha mfumo unafanya kazi bila matatizo.

Kuwepo kwa maafisa wa dawati la msaada kumeondoa kikwazo cha umbali kwa waombaji. Waombaji hawakuhitaji kwenda ofisi za Bodi walipokuwa wanakumbana na matatizo wakati wa kujaza fomu; badala yake walihitaji kutumia simu za mkononi. Waombaji wa mikopo wa ndani na nje ya nchi waliweza kusaidiwa.

Bodi ilitoa muda wa kutosha kwa waombaji wa mara ya kwanza kuomba mikopo, na kwa Wanafunzi wanaoendelea na masomo kuhakiki taarifa zao. Mzunguko wa maombi ya mkopo kwa mwaka wa masomo 2012/2013 ulianza Aprili 16, 2012 mpaka Juni 30, 2012. Baadhi ya Wanafunzi wanaoendelea na masomo hawakuthibitisha taarifa zao ndani ya muda lakini walipatiwa majuma manne zaidi kuhakikisha wanahakiki taarifa zao iwapo walitaka kuendelea kupatiwa mkopo au la.

Dawati la msaada pia lilifanya kazi katika ofisi za kanda Dodoma na Zanzibar kuhakikisha kwamba mfumo wa kuomba mikopo ulikuwa unafanya kazi ipasavyo kwa kuwasaidia Wanafunzi waliokuwa wanakumbana na matatizo ya kiufundi.

# Uendelevu wa Mikopo ya Wanafunzi Nchini Tanzania



*Maafisa wa Madawati ya Mikopo katika Taasisi za Elimu ya Juu wakiwa katika picha ya pamoja baada ya ufunguzi rasmi wa mkutano na Bodi uliofanyika Oktoba 11, 2012 katika Hoteli ya Blue Pearl, Ubungo Plaza, Dar es Salaam.*

NA DAUD MANENO

Tangu mwanzoni mwa miaka ya 1990, mikopo ya Wanafunzi imechukuliwa kama njia muafaka ya kuchangia gharama ya elimu ya juu duniani kote. Uchangiaji wa gharama kama sera inayopendwa; inahitaji kupata vyanzo mbadala vya ugharamiaji ili kupanua upatikanaji wa elimu kwa vile wanafunzi wanahitaji kuchangia kwa kuzingatia faida binafsi wanayoipata katika elimu yao, kama ambavyo Serikali inachangia kwa kuzingatia faida kwa umma. Kwa hali hiyo, katika kipindi cha miongo miwili iliyopita, mifuko mingi ya kugharamia wanafunzi wa elimu ya juu imeanzishwa duniani kote, na hasa katika nchi zinazoendelea na zenye kipato cha kati.

Kwa vile mifumo hii ya mikopo imeenea katika nchi zinazoendelea, ni wazi kwamba mafanikio ya mikopo hii katika nchi zinazoendelea yamelenga katika sababu ambazo hazitumiki katika nchi nyingi zilizoendelea. Sababu moja muhimu kati ya hizo ni mifumo inayowaruhusu wakopaji kutafutwa na kupatikana moja kwa moja kupitia mifumo ya kodi; hata mahali ambapo hilo haliwezekani, uwepo wa ofisi zinazoshughulika na takwimu za mikopo au vitambulisho vya taifa, vimewezesha wakopaji kutafutwa na kupatikana kwa ajili ya kurejesha mikopo.

Sera ya uchangiaji wa gharama za huduma za jamii ikiwemo elimu ya juu, ilianza kutumika nchini Tanzania mnamo mwaka 1992; lengo lilikuwa kuboresha utoaji wa huduma za jamii kwa wahitaji na hivyo kupunguza mzigo kwa Serikali katika utoaji wa huduma hizo.

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ilianzishwa mwaka 2004 kwa Sheria Nambari 9 na kuanza rasmi Julai, 2005 ikiwa ni taasisi inayojitegemea. Kulingana na Sera ya Taifa ya Elimu ya Juu ya 1999, Sheria ya kuanzisha Bodi ilitungwa ili kuwasaidia Wanafunzi wahitaji na pia Bodi hiyo ikusanye fedha za mikopo yote iliyotolewa kwa wanafunzi kuanzia mwaka 1994 na kufanya ukopeshaji wanafunzi kuwa endelevu. Kuanzishwa kwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ilikuwa ni awamu ya tatu ya utekelezaji wa Sera ya Uchangiaji hapa nchini.

Tangu kuanzishwa kwake na baadaye kuanza rasmi shughuli za utendaji, Bodi imefanikiwa kutoa mikopo kwa idadi kubwa ya Wanafunzi ikilinganishwa na hali ilivyokuwa kabla Bodi haijaanzishwa. Mnamo mwaka 2005/2006 Bodi ilitoa mikopo kwa Wanafunzi **42,729** wa elimu

**endelea uk. 8**

# Uendelevu wa Mikopo...

ya juu. Idadi ya Wanafunzi wanaopewa mikopo imeendelea kuongezeka kutoka wanafunzi **58,798** mwaka 2008/2009 hadi Wanafunzi **92,791** mwaka 2010/2011 na kuongezeka zaidi kufikia Wanafunzi **94,533** katika mwaka wa fedha 2011/2012. Hii ni sawa na ongezeko la wastani kwa mwaka la **10.4%.** Mikopo iliyotolewa kwa Wanafunzi wahitaji iliongezeka kutoka **Tzs 56.1 Bilioni** mwaka 2005/2006 hadi **Tzs 310.9 Bilioni** mwaka wa fedha 2011/2012. Hata hivyo, idadi ya Wanafunzi wanaodahiliwa katika Taasisi za Elimu ya Juu imeongezeka kutoka Wanafunzi **40,993** mwaka 2005/2006 hadi wanafunzi **140,918** mwaka 2010/2011; hii ikiwa ni sawa na ongezeko la mwaka la **15.1%.** Ongezeko hili la Wanafunzi wanaodahiliwa katika Taasisi za Elimu ya Juu linaleta changamoto kwa Bodi kukidhi mahitaji ya mikopo ikilinganishwa na raslimali zilizopo.

Hadi sasa Bodi bado inategemea Serikali kwa kiasi kikubwa, kama chanzo kikuu cha mikopo kwa wanafunzi. Chanzo kingine ni urejeshaji mikopo ambao mwenendo wake unaridhisha ingawa bado unakabiliwa na ugumu fulani, baadhi yake ikiwa ni changamoto ya kuwatafuta wanufaika; kutokuwepo kwa ushirikiano wa kutosha kutoka kwa waajiri na kutokuwepo kwa utamaduni wa kurejesha mikopo miongoni mwa wanufaika wa mikopo.

Kwa kifupi inaweza kuelezwa kwamba viwango vidogo vya urejeshaji mikopo vinatokana na ugumu wa kuwapata wanufaika wa mikopo, kiwango cha riba kiko chini sana, muda wa kusubiri kabla ya kurejesha mikopo (grace period) na vipindi vya kurejesha mikopo ni virefu mno bila sababu. Mwisho, upatikanaji mdogo wa ajira katika uchumi wa nchi za Afrika na uwezo usio sawa wa kujiajiri katika maeneo ya vijijini na pembezoni mwa miji katika nchi nyingi zinazoendelea; vyote ni changamoto kwa uwezo wa wanufaika wa mikopo kurejesha mikopo hiyo ambayo vinginevyo ingekopeshwa tena kwa Wanafunzi wahitaji.

Kwa ujumla, ukosefu wa ajira unazaa matatizo mengi ya kijamii ambayo yanachangia wanufaika wa mikopo kupoteza uaminifu wa kurejesha mikopo yao kutokana na ukweli kwamba hawana kipato. Kwa vile ukosefu wa ajira nchini Tanzania ni kitu cha kawaida na unaendelea kuongezeka kadri siku zinavyosonga mbele, ufanisi wa Bodi katika kukusanya mikopo ya Wanafunzi unaathiriwa na hivyo kukwamisha utoaji mikopo endelevu.

Pamoja na yote haya, Bodi inaendelea kuimarisha mikakati ya kuboresha viwango vya urejeshaji mikopo ambapo kwa sasa ni 54% ya mikopo ambayo imeiva kwa ajili ya kurejeshwa ili ifikie **70%** kufikia Juni, 2014.

# DONDOO ZA KUVUTIA

1. Je unajua kwamba, katika mwaka wa fedha 2012/2013, waombaji wa mikopo wa mara ya kwanza wamepewa mikopo kulingana na uhitaji- mbinu ya uchambuzi wa mikopo ambayo ni rahisi, yenye usawa na ya wazi!
2. Je unajua kwamba katika mwaka wa masomo 2012/2013, kiasi cha **71.35%** ya waombaji mikopo wa mara ya kwanza wa 2012/2013 walipangiwa mikopo baada ya kubainika kuwa wana uwezo wa kuchangia chini ya **Tzs 500,000.00** kwa mwaka kwa ajili ya elimu ya Chuo Kikuu, wakati **15.23%** ni wale ambao wanaweza kuchangia kati ya **Tzs 500,000.00** na **Tzs 1,000,000.00** kwa mwaka!
3. Je unajua kwamba katika mwaka wa fedha 2012/2013 kiasi cha **70.08%** ya waombaji mikopo wa mara ya kwanza waliopata mikopo wamedahiliwa kujiunga na Kozi za kipaumbele? Kati yao **45.75%** wamedahiliwa katika Ualimu wa masomo yasiyo ya Sayansi; wakati kozí zingine za kipaumbele (Sayansi za Afya, Ualimu wa Hisabati, Ualimu wa masomo ya Sayansi, Sayansi za Kilimo, Sayansi za Wanyama na Uhandisi wa Umwagiliaji) ni **24.37%** ya Wanafunzi wote waliopata mikopo kwa mara ya kwanza. Halikadhalika, kozí za Sayansi ni **5.89%** na kozí zingine (zisizo za kipaumbele) ni **24.02%** tu ya Wanafunzi wote wa mwaka wa kwanza waliopangiwa mikopo!
4. Je unajua kwamba, kuna mipango ya kuwafikisha wadaiwa sugu wa mikopo kwenye Ofisi ya Takwimu za wakopaji ili wazuiwe kupata mikopo mingine!
5. Je unajua kwamba wadaiwa sugu wa mikopo sasa wanatozwa faini **10%** ya kiwango cha mkopo wanachopaswa kurejesha?
6. Je unajua kwamba kiwango cha makato ya mikopo ni **8%** ya mshahara au mapato mengine ya mwezi?

# Kupandishwa Vyeo na Uhamisho wa Wafanyakazi

NA ELINE MARONGA













**1 Bw. Josephat T. Bwathondi**

**2 Bw. Saleko F. Mandara**

**3 Bi. Sarah D. Fihavango**

**4 Bw. Leonard Mcharo**

Katika kutambua uchapakazi na nidhamu, wafanyakazi wanne wa Bodi wamepandishwa vyeo. Wafanyakazi hao wamepandishwa vyeo kutokana na ufanisi katika kazi zao. Baadhi yao walipandishwa vyeo na kuhamishiwa katika Vitengo ama Idara nyingine ili kuongeza ufanisi na kuboresha huduma kwa wateja.

Bw. Josephat T. Bwathondi amepandishwa cheo na kuwa Afisa Mikopo Mwandamizi katika Kitengo cha Uchambuzi wa Mikopo. Kabla ya kupandishwa cheo, alikuwa Afisa Mikopo. Ana furaha na anaamini anaendelea kukua kiweledi na uzoefu kazini. Bw. Bwathondi alisema, nafasi hiyo mpya imemfanya aongeze jitihada na kuwa na hamu ya kujifunza vitu vingi zaidi ambavyo vitanufaisha Kitengo chake na halikdhalika Bodi kwa ujumla. Pia anaamini katika ubunifu na kuwa na mawazo mapya kwa ajii ya kuboresha Kitengo cha Uchambuzi wa Mikopo.

Alipoulizwa kuhusu changamoto zinazoambatana na majukumu yake, alibainisha kujifunza miundo ya mfumo wa uchambuzi wa mikopo kuwa ni changamoto na kwamba muda wa kutosha unahitajika ili kuufahamu mfumo huo mpya. Halikadhalika anafikiria kwamba, mafunzo kazini kuhusu jinsi ya kuwahudumia wateja, mfumo na takwimu za msingi vitasaidia kuongeza ujuzi wake ili ájese kuwa na ufanisi zaidi.

Bw. Saleko F. Mandara ambaye alikuwa Afisa Urejeshaji Mikopo pia amepandishwa cheo. Hivi sasa anafanya kazi katika nafasi ya Afisa Mwandamizi wa Utoaji Mikopo. Alihamishwa kutoka Idara ya Urejeshaji Mikopo kwenda Idara ya Uchambuzi na Utoaji Mikopo akifanya kazi katika Kitengo cha Utoaji Mikopo. Akizungumzia mabadiliko hayo alisema; "mwanzoni ilikuwa ni changamoto kufanya kazi mpya tofauti na zile nilizokuwa nimezizoea, lakini baada ya muda nimezoea na najisikia vizuri kufanya kazi yangu mpya. Mwanzoni nilikuwa nashughulikia wanufaika wa mikopo ambao tayari wameshahitimu lakini sasa nahudumia Wanafunzi ambao wanahitaji mikopo ili waweze kupata elimu ya juu." Aliongeza kusema kwamba, amejitoa zaidi kuhakikisha anaifanya kazi yake vizuri zaidi.

Bi. Sarah D. Fihavango amepandishwa cheo na kuwa Afisa Mikopo Mwandamizi wa Utoaji Mikopo. Kabla ya kupandishwa cheo alikuwa Afisa Utoaji Mikopo. Akitoa maoni jinsi gani anaweza kufanya kazi zake pamoja na kuwasimamia maafisa wa chini yake, Bi. Fihavango alisema; " ni kazi inayohamasisha na kuleta changamoto. Ilinichukua muda kidogo kuwaelewa wafanyakazi walio chini yangu kwa vile wengi wao walikuwa waajiriwa wapya. Kwa sasa nawafahamu vizuri na hii inaniwezesha kufanya nao kazi kwa urahisi zaidi". Pia anaamini kwamba, kwa nafasi hiyo mpya anapanua uelewa na kuongeza ujuzi wake. Alipendekeza kwamba, mafunzo ya Mfumo wa Utoaji Mikopo na hasa kwa wafanyakazi walio chini yake yawepo ili kuwapatia ujuzi wa kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi.

Bw. Leonard Mcharo ambaye awali alikuwa Afisa Urejeshaji Mikopo katika Idara ya Urejeshaji Mikopo, amepandishwa cheo kuwa Afisa Mikopo Mwandamizi katika Idara ya Uchambuzi na Utoaji Mikopo. Anafanya kazi katika kitengo cha Uchambuzi wa Mikopo. Akizungumzia jinsi anavyoiona kazi yake mpya, anabainisha kuwa mwanzoni ilikuwa ni changamoto kubwa ikizingatiwa kwamba hakuwa na uzoefu na kazi za uchambuzi wa mikopo lakini sasa anafurahi ameweza kujifunza kwa haraka. "Naifurahia kazi yangu", alisema. Anapendekeza kwamba mfumo wa urejeshaji mikopo uboreshwe zaidi ili kurahisisha utoaji wa huduma na hatimaye kuwapata wanufaika kwa urahisi.

# Menejimenti ya Bodi Yakaribisha Wafanyakazi Wapya

NA JOYCE MGAYA NA SUNDAY CHARLES

Bodi imeajiri wafanyakazi wapya 20 ili kuboresha utoaji huduma. Hatua hii ililenga kuimarisha Idara na Vitengo vilivyopo katika kukabiliana na ongezeko la mahitaji ya wateja wake. "Tumeamua kuajiri wafanyakazi wapya vijana na wenye nguvu ili kuwaongeza katika timu yetu tuweze kuinua uwezo wa Bodi katika kuwahudumia wateja wake", alisema Bw. George Nyatega, Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi.

Katika hotuba yake ya ukaribisho, Mkurugenzi Mtendaji alitoa wito kwa wafanyakazi wapya kuwa na bidii na uadilifu katika kipindi watakachofanya kazi Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu na akaongeza kuwa mafanikio ya Bodi yanategemea uwezo wao wa kufanya kazi kwa bidii huku wakizingatia tunu kuu zinazothaminiwa na Bodi.

Alisema, Bodi ilich ukua uamuzi muhimu wa kuajiri wafanyakazi vijana kwa imani kwamba wataleta mawazo mapya na ubunifu katika utendaji wa Bodi. Aliongeza kwamba Menejimenti ilichagua kuwekeza katika wafanyakazi wapya na kuwapa mafunzo ya mwezi mmoja ili kuwapa fursa ya kujifunza na kuzoea utendaji wa kila siku na hatimaye waweze kuleta mchango chanya kwa shirika.

Mafunzo hayo ya mwezi mmoja yalijumuisha vipindi vya kufundishwa miongozo 14 ya utendaji inayotumiwa na Idara na Vitengo vya Bodi katika shughuli zake za kila siku, vipindi vya maswali na majibu, mafunzo kwa vitendo na mwisho marudio na majaribio ya vipindi vyote walivyofundishwa.

Vipindi vya mafunzo viliendeshwa na wakuu wa Idara na Vitengo na pia maafisa kadhaa wa serikali

**endelea uk. 11**

## Kumbukumbu ya Voster Prosper Mariki

NA SUNDAY CHARLES



Mei 24, 2012, ni siku ambayo wafanyakazi wengi wa Bodi hawataisahau kwa urahisi. Ni siku ambayo walimpoteza rafiki na mwenzao, Voster Prosper Mariki.

Marehemu Mariki alifariki dunia katika Hospitali ya Taifa Muhimbili alikokuwa amelazwa kwa matibabu.

Mariki alijiunga na Bodi mnamo Julai 2, 2007 akiwa Dereva Daraja II, na kutokana na kujitoa na kufanya kazi kwa bidii. Mnamo Julai, 2010 alipandishwa cheo na kuwa Dereva Daraja I, nafasi ambayo alikuwa nayo hadi mauti yalipomfika.

Hakuna Maneno yanayoweza kueleza ni kwa kiasi gani atakumbukwa na familia yake, ndugu na wenzake wa karibu aliofanya nao kazi Bodi kwa vile alikuwa bado kijana mwenye nguvu na mengi yalitarajiwa kutoka kwake.

"Nilikutana na Mariki nilipojiunga na Bodi mwaka 2007, tangu wakati huo amekuwa rafiki yangu mkubwa na rafiki wa watu wengine hapa Bodi" alisema Bw. Phillip Urio, rafiki wa karibu wa Mariki.

Akitoa salamu za rambirambi katika ibada ya mazishi, Mkurugenzi Msaidizi wa Raslimali Watu na Utawala, Bw. Gabriel Rhobi kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji alisema kifo cha Mariki ni pigo kwa Bodi.

"Alikuwa mchapa kazi, na aliitumikia Bodi katika nafasi ya Dereva kwa uaminifu mkubwa na nia ya dhati", alisema Bw. Rhobi.

Marehemu Voster Prosper Mariki alizaliwa Oktoba 10, 1968, katika Manispaa ya Mbeya. Alipata elimu ya msingi katika Shule ya Msingi Sisimba kuanzia 1977 hadi 1983 na baadaye akajiunga na Shule ya Sekondari Sangu mnamo mwaka 1984 na kuhitimu 1987.

Mariki alihudhuria mafunzo mbalimbali kama vile mafunzo katika Chuo cha Usafirishaji cha Taifa (NIT) na 2011 alitunukiwa cheti cha Udereva wa Viongozi.

Marehemu Mariki alifunga ndoa na Bi. Doreen Eliyona Moshi Desemba 25, 1999 jijini Dar Es Salaam, na walijaaliwa kupata watoto watano.

ROHO YAKE IPUMZIKE KWA AMANI. AMINA.

**inatoka uk. 10**

walioalikwa kutoka Serikali Kuu. Mafunzo yaliratibiwa na Mkurugenzi Msaidizi wa Raslimali Watu na Utawala (ADHRA) ambaye katika muda wote wa mafunzo alisisitiza juu ya wajibu wa mtumishi wa umma katika kuheshimu maadili, sheria na kanuni za kazi.

Siku ya mwisho ya mafunzo, Mkurugenzi Mtendaji alikutana na wafanyakazi wapya na akaelezea matumaini na matarajio ya Menejimenti kwao. Katika hotuba yake ya kufunga mafunzo, Mkurugenzi Mtendaji alisema kuwa alikuwa na imani kwamba mafunzo hayo yaliwasaidia wafanyakazi wapya kufahamu utendaji kazi wa kila siku wa Bodi na kuwashauri kufanya kazi kulingana miongozo ya utendaji.

Alisema Bodi ina nia ya kuwapa mafunzo wafanyakazi wake ili kuboresha ufanisi na ujuzi wao wa kazi na kwamba mafunzo ya aina hiyo yanahitajika ili kuongeza ubora wa huduma zinazotolewa na shirika kwa wateja wake na wakati huo huo kuwawezesha kujenga uwezo na weledi wa kila mfanyakazi.

Akitoa shukrani kwa Menejimenti kwa niaba ya wafanyakazi wenzake wapya, Bw. Godfrey Chawe (Afisa Mikopo) alisifu jitihada za Menejimenti katika kushiriki moja kwa moja kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wapya. Aliahidi kuweka jitihada na nguvu zake katika kufanya kazi alizopangiwa.



*Mwenyekiti wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Prof. Anselm Lwoga akitambulishwa kwa wafanyakazi wa Ofisi ya Bodi ya Kanda Dodoma alipotembelea ofisi hiyo Novemba 20, 2012. Anayetambulisha wafanyakazi ni Meneja wa Kanda Dodoma Bw. Chikira Jahari.*

































1 *Mwenyekiti wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Prof. Anselm Lwoga akitambulishwa kwa wafanyakazi wa Ofisi ya Bodi ya Kanda Dodoma alipotembelea ofisi hiyo Novemba 20, 2012. Anayetambulisha wafanyakazi ni Meneja wa Kanda Dodoma Bw. Chikira Jahari.*

2 *BBaadhi ya wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Bodi wakishiriki katika mkutano uliofanyika Oktoba 20, 2012 katika Hoteli ya Oceanic Bay Resort, Bagamoyo.*

3 *Wajumbe wa Kamati ya Jinsia na Huduma za Jamii ya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar wakimsikiliza Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi Nd. G.R.W.Nyatega. Kamati ilifanya ziara hiyo tarehe 6 Machi, 2012.*

4 *Mkuu wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Dkt. John Magoti (kulia) katika picha ya pamoja na maafisa wa Bodi walipotembelea Taasisi hiyo.*

5 *Sehemu ya ujumbe wa Wabunge kutoka Uganda wakimsikiliza Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (hayupo pichani) walipokuwa katika ziara ya Mafunzo kuanzia Novemba 15 hadi 16, 2012.*

6 *Mwenyekiti wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Prof. Anselm Lwoga akisaini kitabu cha wageni katika Ofisi ya Bodi ya Kanda Dodoma Novemba 20, 2012.*

7 *Washiriki wa Mafunzo juu ya urejeshaji mikopo wakiwa katika picha ya pamoja na Wakufunzi siku ya mwisho ya mafunzo hayo. Waliokaa (Watatu kutoka kushoto) ni Nd. Benjamin C. Cheboi, aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Mikopo ya Kenya. Kushoto kwake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mikopo (HESLB) Nd. George R.W. Nyatega.*

8 *Mkutano wa pamoja kati ya Bodi na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) uliofanyika Agosti 10, 2012. Wa pili kutoka kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Prof. Anselm Lwoga na wa pili kulia na Kaimu Mkuu wa Chuo hicho Bw. Athman Ahmed.*

9 *Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Nd. Celestine Gesimba akiwa katika picha ya pamoja na wajumbe wa mkutano wa nusu mwaka wa AAHEFA, uliofanyika kwenye Hoteli ya Snow Crest, Arusha tarehe 27 - 28 Septemba, 2012.*

10 *Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Bodi wakipiga picha ya pamoja kabla ya kuanza mkutano wao Oktoba 20, 2012.*